

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na.HW/W:20/70/19




05/11/2021

TANGAZO KWA WATUMISHI WOTE.

Serikali kupitia sera yake ya kuboresha maisha ya watumishi wake imeamua kutoa mikopo kwa watumishi wa serikali za Mitaa kwa ajili ya ununuzi wa Magari, Samani, matengenezo ya Magari na Pikipiki. Serikali imetoa kiasi cha Tshs. 250,000,000/= kwa ajili ya mkopo huo.

Kwa tangazo hili Watumishi wote mnakaribishwa kutuma maombi kwa ajili ya mkopo tajwa hapo juu kwa masharti yafuatayo:

- Mkopo utatolewa kwa mtumishi mwenye Ajira ya Masharti ya Kudumu.
- Mkopo utatolewa kwa Mtumishi aliyethibitishwa kazini.
- Mkopaji anatakiwa kubakiwa na 1/3 ya mshahara wake baada ya makato ambayo yatarejeshwa kwa kipindi kisichozidi miezi 72 (miaka 6).
- Mkopaji anatakiwa kutuma barua ya maombi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kupitia kwa Mkuu wake wa Idara na Mkuu wake wa Kituo.
- Barua ya maombi iambatishwe na nakala ya Barua ya Ajira, Barua ya kuthibitishwa kazini, na hati ya Mshahara ya mwisho.
- Mikopo hii hainunui deni kutoka taasisi nyingine za fedha.
- Mkopaji atalipa "Service charge" 3% na Protect fund 1% kutoka kwenye mkopo atakaokopa.
- Mkopo unaotolewa kwa mtumishi hauna riba
- Mkopo utatolewa kwa mtumishi mwenye mwenendo mzuri kazini na utendaji mzuri wa kazi katika Utumishi wa Umma.
- Mkopo huu hautatolewa kwa mtumishi aliyekwisha nufaika (**ana marejesho ya mkopo wa Serikali kwenye Salary Slip yake**).
- Fomu za maombi zinapatikana ofisi za Masjala ya Mkurugenzi Mtendaji (W) pamoja na kwenye website ya Halmashauri (www.bundadc.go.tz)
- Mwisho wa kupokea maombi ya mkopo huu ni tarehe 19/11/2021


Changwa M. Mkwazu
Mkurugenzi Mtendaji (W)
RINDA

VIWANGO VYA MIKOPO


AINA YA MKOPO	NGAZI YA MKOPO	KIWANGO CHA JUU CHA MKOPO	MUDA WA MAREJESHO
Mkopo Taslimu kwa ajili ya Ununuzi wa Magari, Pikipiki, Samani na matengenezo ya vyombo vya usafiri.	TGS A-C TGTS A-C TGHS A-C TGOS A-C TGHOS A-C	Milioni 15,000,000/=	Miezi 72 (Miaka 6)
	TGS D-F TGTS D-F TGHS D-F	Milioni 30,000,000	Miezi 72 (Miaka 6)
	TGS G-H TGTS G-H TGHS G-H	Milioni 40,000,000/=	Miezi 72 (Miaka6)
	LSSE I-4 TGTS I TGHS I-J	Milioni 50,000,000/=	Miezi 72(Miaka 6)

Fomu za maombi zinapatikana ofisi ya Masijala ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Mkopaji anatakiwa kutuma maombi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kupitia kwa Mkuu wake wa Idara na Mkuu wake wa kituo na anapaswa kuambatanisha fomu ya maombi nakala ya Barua ya Ajira, Barua ya kuthibitishwa kazini, hati ya Mshahara wa mwisho (salary slip) pamoja na passport size 2. Maombi yanapaswa kuwasilishwa ofisi ya Masjala iliyopo Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda (Kibara) kwa mkono. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 19/11/2021 saa 9:30 mchana.

Maombi yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Mtendaji (W),
S.L.P 126,
BUNDA.


 Changwa M. Mkwazu
 Mkurugenzi Mtendaji (W)
BUNDA.